

NINAPATAJE MKOPO WA KODI YA MTOTO?

Je, wewe na watoto wako mnaishi nchini Marekani katika mwaka wa 2021 na watoto wako wana nambari za usalama wa kijamii?

Hapana

Huenda usistahiki kupokea mkopo wa kodi ya mtoto.

Ndiyo

Je, uliwasilisha kodi ya mwaka 2020?

Ndiyo

**Je, una mtoto aliyezaliwa
mwaka 2021?**

Hapana

Ikiwa una watoto wengine wanaostahiki, utapokea malipo kiotomatiki kuanzia tarehe 15 Julai, 2021.

Pata taarifa zaidi hapa:
<https://www.irs.gov/credits-deductions/advance-child-tax-credit-payments-in-2021>

Ndiyo

Hapana

Ikiwa hukuwasilisha kodi, utahitaji basi kujulisha IRS kuhusu watoto wako wanaostahiki kupitia zana yao ya kujisajili: <https://www.irs.gov/credits-deductions/child-tax-credit-non-filer-sign-up-tool>

Ndiyo

Hongera! Mara tu mtoto wako anapokuwa na nambari ya usalama wa kijamii unaweza kujisajili ili kuanza kupokea malipo ya mkopo ya kila mwezi ya mtoto.

<https://www.irs.gov/credits-deductions/child-tax-credit-update-portal>

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

Ikiwa nitajisajili kwa Mkopo wa Kodi ya Mtoto, itaathiri marupurupu yangu mengine ya serikali (kama SSI, SNAP, TANF au WIC)?

Hapana. Kupokea malipo ya Mkopo wa Kodi ya Mtoto hakuzingatiwi kuwa mapato kwa familia yoyote. Kwa hivyo, haitabdalisha kiwango unachopokea katika marupurupu mengine ya Shirikisho. Marupurupu haya ya Shirikisho ni pamoja na bima ya ukosefu wa ajira, Medicaid, SNAP, SSI, SSDI, TANF, WIC, Section 8 au Makazi ya Umma.

 **General Assistance inaweza kuathiriwa!** Ikiwa uko kwenye General Assistance, unaweza kuchagua kujiondoa kwa malipo ya kila mwezi kwa sababu yoyote. Ili kujiondoa kwa malipo ya kila mwezi, au kuondoa usajili wako, unaweza kwenda kwa Tovuti ya Sasisho la Mkopo wa Kodi ya Mtoto ya IRS. Ikiwa unachagua kutopokea malipo ya kila mwezi, utapata Mkopo kamili wa Kodi ya Mtoto kama mkupuo mwaka ujao unapowasilisha malipo yako ya kodi: <https://www.irs.gov/credits-deductions/child-tax-credit-update-portal>

IRS itatuma pesa yangu wapi?

IRS itatuma malipo yako kwa amana ya moja kwa moja kwenye akaunti ya benki waliyo nayo kwenye faili. Ikiwa hawana taarifa ya akaunti yako ya benki, hundi itatumwa kwako.

Je, itakuwaje ikiwa sina nambari ya usalama wa kijamii lakini mtoto wangu anayo?

Ikiwa huna Nambari ya Usalama wa Kijamii, unaweza kutumia ITIN (Nambari ya Kitambulisho cha Mlipa Kodi). Unaweza kupata ITIN kwa kujaza Fomu ya W-7 na IRS. Tazama <https://www.irs.gov/individuals/how-do-i-apply-for-an-itin>

Nitapokea kiasi gani katika malipo ya Mkopo wa Kodi ya Mtoto?

Familia nyingi zitapokea kiasi kamili: \$3,600 kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka 6 na \$3,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa miaka 6 hadi 17. Ili kufikisha pesa kwa familia mapema, IRS itatumia familia nusu ya Mkopo wa Kodi ya Mtoto wa 2021 kama malipo ya kila mwezi ya \$300 kwa kila mtoto chini ya umri wa miaka 6 na \$250 kwa mtoto kati ya umri wa miaka 6 na 17.

Kiasi hiki kinawenza kutofautiana kulingana na mapato. Watu hawa wanastahiki Mkopo kamili wa Kodi ya Mtoto:

- Wanandoa walio na mapato ya chini ya \$150,000
- Familia zilizo na mzazi mmoja (pia huitwa Kichwa cha Familia) aliye na mapato ya chini ya \$112,500
- Kila mtu mwingine mwenye mapato ya chini ya \$75,000

Watu hawa watastahili kupata angalau \$2,000 ya Mkopo wa Kodi ya Mtoto, ambao huwa \$166 kwa kila mtoto kila mwezi:

- Wanandoa walio na mapato ya chini ya \$400,000
- Familia zilizo na mzazi mmoja (pia huitwa Kichwa cha Familia) aliye na mapato ya chini ya \$200,000
- Mtu mwingine ye yote aliye na mapato ya chini ya \$200,000

Familia zilizo na mapato ya juu zaidi zinawenza kupokea kiasi kidogo au kutopata mkopo kabisa.

Pata maelezo zaidi: www.whitehouse.gov/child-tax-credit/

Je, unahitaji msaada wa kulipia au kupata huduma ya utunzaji wa watoto hu ko Portland Maine? Pata maelezo zaidi hapa: www.portlandofopportunity.com/how-do-i-find-childcare